Presec?, Private Secy.

# JAMHURI YA TANGANYIKA

STATE HOUSE 23 SEP 1963 DAR ES SALAAM

# ELIMU

## KATIKA 1963 NA 1964

UHURU NA UMOJA



Bwana S. N. Eliufoo
Waziri wa Elimu

INATOLEWA BURE NA IDARA YA HABARI

No. I

# Hotuba ya Waziri wa Elimu katika Bunge Juni 1963

Bwana Hatibu, naomba kutoa azimio kuwa sasa uondoke katika Kiti, ili iwepo nafasi ya majadiliano juu ya shabaha ya mpango wa elimu uliyomo katika makadirio ya fedha ya Wizara ya Elimu.

Ingawaje mwezi Desemba mwaka wa jana, nilijitua mzigo wa Uenezaji wa habari, utangazaji wa habari, uchunguzi wa picha za sinema, usimamizi wa mambo ya uhalifu ya vijana na mambo ya michezo na uhifadhi wa mambo ya sanaa, Wizara yangu bado ni mojawapo ya wizara zilizo kubwa sana, na hutumia sehemu iliyo kubwa sana ya fedha zilizokadiriwa kwa nchi nzima.

Huu umekuwa mwaka wa kusisimua, na napenda kutoa mipango ya mwaka ujao kwa kulinganisha na mafanikio yetu mbali mbali ya mwaka huu. Bwana Hatibu, watu mara nyingi huona uchovu kuonyesha mambo yao kwa hesabu kamili. Hata hivyo naazimia kuanza kwa kuwapa hesabu chache, kwa sababu hesabu kamili zinazoonyesha maendeleo mara nyingi ni tamu kuzisikiliza, na hesabu hizi nitakazowapeni, zaonyesha maendeleo tuliyoyafanya katika miezi kumi na miwili iliyopita katika kutoa nafasi zaidi kwa watoto shuleni

**Miaka mitatu iliyopita, idadi ya watoto walioandikishwa katika darasa la kwanza ilikuwa ni 116,600; leo idadi hiyo ni 170,000. Wakati huo huo, idadi ya watoto walioandikishwa katika darasa la V imeongezeka mara mbili kutoka 17,500 mpaka 32,000. Katika darasa la IX (Form I) hesabu imeongezeka kutoka 3,643 mpaka 5,000, na katika darasa la XIII (Form V) imeongezeka kutoka 200 mpaka 518. Wale wanaosoma katika vyuo vya juu vilivyo nje ya Afrika ya Mashariki, hesabu yao imeongezeka toka 1,306 mpaka 1,500. Katika wakati huu huu kumekuwa na maongezeko ya watu 250,000 wanaopata masomo.**

### Mambo ya kusisimua —Mkuu wa kwanza wa Chuo Kikuu

Kabla sijaingilia mambo mengi, ningependa kugusia mambo makubwa ya mwaka huu-ule ukaguzi wa wataalamu wa UNESCO juu ya mipango ya maendeleo na ile ripoti yao nzuri, mipango ya kuwa na Kundi Moja la Waalimu (Unified Teaching Service) ambalo sasa lina ofisi yao na wafanyaji kazi wake, kule kuongezeka kwa idadi ya Waafrika wenye kazi za madaraka, mikutano miwili ya Halmashauri ya Elimu (Advisory Council on Education) mipango ya kusisimsha ya kuongeza elimu kwa mipango ya kujenga taifa, majengo ya kwanza ya Chuo Kikuu Cha Elimu Dar es Salaam huko Ubungo, na mwishowe kuchaguliwa kwa Rais wetu kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afrika ya Mashariki.

Bwana Hatibu, Wizara hii ni kubwa na hutumia fedha nyingi. Imegawanyika, kwa madhumuni ya kazi, katika sehemu mbali mbali, na kwa ruhusa ya waheshimiwa wote wa nyumba hii nitaonyesha kazi ya kila sehemu.

### Mafunzo ya ualimu

**Mafunzo ya ualimu ndio msingi wa kila mpango wa elimu katika nchi yoyote, na nakusudia kuzungumza juu ya Mafunzo ya Ualimu kabla sijazungumza juu ya shule zetu. Bado hatujawa na waalimu wa kutosha wenye vyeti vinavyohitajika hasa kwa mafunzo ya elimu ya juu. Hata hivyo sijui kama iko nchi yoyote ulimwenguni ambayo imejitosheleza katika jambo hili. Tunakusudia kuwapata waalimu wetu kwa njia tatu-kwa kuwafundisha wanafunzi toka shuleni na hata kutoka watu ambao walikuwa wafanya kazi nyinginezo, kwa mipango ya kuwapatia waalimu mafunzo ya kuinua elimu yao (Upgrading Courses), na kwa kuwaajiri walimu kutoka nchi za ng'ambo kwa njia ya misaada toka nchi za nje.**

Jitihada kubwa lazima ifanywe na sisi wenyewe hapa Tanganyika, na napenda kuvishukuru vyama mbali mbali vya dini kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya kila wakati kwa kufundisha na kutoa walimu toka vyuo vyao kwa faida ya nchi nzima.

Mpango wa Elimu wa Miaka mitatu ulikusudia kuongeza idadi ya Waalimu wa daraja la 'C' mpaka 725 kila mwaka, na kuongeza idadi ya waalimu wa daraja la 'A' mpaka 225 kwa mwaka. Mpango uliohitajika wa kupanua vyuo vyetu vya kufunzia waalimu umekwisha malizika na kukamilika, bali idadi ya waalimu iliyotajwa hapo juu haitaonekana mpaka mwisho wa 1964. Kusudio letu kwa hivyo karibu limetimilizwa.



Hii ni sehemu tu ya majengo ya Chuo Kikuu cha Tanganyika, kinachojengwa huko sehemu ya Ubungo, karibu ya Dar es Salaam.

kwa muda. Kwa ufupi, mambo makuu katika mpango wa kuamua ubora wa digrii kwa sasa ni haya:

**(a) Jambo kubwa hasa ni muda wa kupata elimu, kama inavyoweza kulinganishwa na muda ule wa elimu ambayo humpatia mtu digrii katika Chuo Kikuu cha Afrika ya Mashariki.**

**(b) Kutambulikana kwa mara moja kwa digrii kuwe ni kwa digrii zile za Vyuo Vikuu ambavyo vimo katika orodha ya Vyuo vya Amerika ambavyo ni sawa na vya Madola.**

**(c) Katika mambo yanayohusu utaalam wa kazi, Wizara huongozwa na mawaidha yenye haki ya wataalam wa kazi inayohusika.**

**(d) Katika majifunzo mengine ambayo hayaamuliki sawasawa kwa vipimo vilivyo juu, kila shauri huchunguzwa kipekee.**

## Pauni milioni tano kwa elimu

Nimezungumza kwa kirefu juu ya mambo mengi. Sasa nataka kutaja yale mambo mengine makubwa na yenye maana sana. Wizara yangu imekisia matumizi ya kawaida (recurrent expenditure) ya kiasi chini kidogo ya pauni 5,000,000. Hiki ni kima kikubwa sana kwa sisi hapa Tanganyika na ni zaidi ya sehemu moja kwa tano ya matumizi yote ya kawaida kwa nchi nzima. Baada ya kuondoa kazi fulani ambazo zilikuwa chini ya wizara yangu, hii huonyesha maongezeko ya pauni 340,000 ukilinganisha na mwaka huu. Sina budi kumshukuru mwenzangu, Waziri wa Fedha, kwa kuniruhusu kutumia kima hiki. Napenda vile vile kuonyesha tumaini langu kuwa baadaye itawezekana kutumia fedha zaidi katika fedha zilizoko nchini kwa mipango ya elimu kwa sababu ya lazima iliyoko ya kupanua elimu kwa upesi kama vile nilivyoshauriwa na ujumbe ule wa Unesco uliochungua mambo ya elimu hapa nchini.

Ingawa kima kikubwa katika maongezeko haya ni kwa elimu ya Sekondari, kwa sababu ambazo nimekwisha kuliambia baraza hili, Wizara yangu bado ingali ikitumia kiasi cha karibu ya nusu ya fedha zake katika elimu ya Primary na kwa njia hii hulipia kiasi cha sehemu 65 kwa mia ya gharama ya elimu ya Primary kwa nchi nzima. Karibu theluthi moja ya fedha zitatumika kwa elimu ya Sekondari, na sehemu hizi mbili za elimu (Primary na Sekondari) pamoja hutumia robo tatu ya matumizi yetu katika wizara ya elimu. Sehemu zinazobakia za wizara ya elimu - elimu ya ufundi (Technical Education), Mafunzo ya Ualimu, Elimu ya Juu, Ukaguzi wa Shule, na kadhalika hutumia robo iliyobakia.

Makadirio yangu ya fedha kwa maendeleo huonyesha matumizi ya pauni 1,575,000. Sehemu moja kwa tatu katika hii ni kwa maongezeko ya shule za Sekondari na theluthi nyingine ya fedha ni kwa Chuo Kikuu (University College). Hizi ni fedha nyingi, na hata hivyo zingeweza kutumia fedha zaidi hata mara mbili ya hiki, na hata hivyo nisingeweza kuridhisha maombi ya watu wa elimu zaidi nchini. Fedha hizi ni chache na hakuna nafasi ya



**Rais, Mwalimu J. K. Nyerere, anaweka jiwe la msingi wa shule ya T.A.P.A. huko Machame karibu ya Moshi.**

kugeuza mipango. Basi ikiwa waheshimiwa wajumbe wa baraza baadaye wakati wa majadiliano haya wataniomba maongezeko zaidi ya shule naweza kuwajibu hivi, 'Onyesha ni wapi katika makisio yangu ya fedha ambapo naweza kupunguza fedha ili kusudi mpango wako uingizwe, na mimi nitakuonyesha ni jambo lipi katika haya mawili ambalo linastahili kutendwa kwanza." Bwana Khatibu, naomba kuwaonya wajumbe kuwa katika kazi ya aina hii wakumbuke kuwa kama umekwisha fungua darasa la IX katika mahali 'A', ni lazima kuendelea na mpanuko mpaka umefikia darasa la XII. Huwezi kuona darasa la X ili kusudi uongeze fedha zilizokadiriwa kwa darasa la XI na XII katika mahali 'B'. Kwa hiyo maombi ya Waheshimiwa nitayaandika mahali fulani na baadaye yatajumlishwa na mipango mingine mingine ambayo ipo katika mpango wetu mpya wa maendeleo.

## Idadi imeongezeka

Je! fedha zote hizi tunazifanyia nini? Idadi ya watoto walioandikishwa darasa la V na la VIII imeongezeka mara mbili katika miaka minne tangu 1959. Idadi ya watoto walioandikishwa katika darasa la I imeongezeka kwa sehemu 25 kwa mia katika shule za Serkali na zile zinazosaidiwa na Serkali, na ukijumlisha na shule zile ambazo hazisaidiwa na Serkai maongezeko ni sehemu 50 kwa mia. Baada ya nchi kujipatia uhuru wake kumekuwa na ari kubwa ya shule hasa shule za Primary. Wakati huo huo idadi ya watoto walioandikishwa katika darasa la XI imeongezeka kwa sehemu 45 kwa mia. Juhudi kubwa sana imeonyeshwa kati ya darasa la X (Form 2) na la XI (Form 3), na hii inaonekana wazi kwa sababu maongezeko ya idadi ya wale wanaomaliza darasa la XII (Form 4) imeongezeka kwa sehemu 280 kwa mia, na idadi hii itaongezeka mwakani kufikia sehemu 300 kwa mia mwaka ujao, ndio mwisho wa mpango wa miaka mitatu.

## Mzigo wa Serikali za Mitaa

Naomba kumaliza hotuba yangu kwa kutaja baadhi ya matumaini yangu kwa wakati ujao. Msingi wa mpango wetu wa elimu ni shule zetu za primary ambazo ni za aina nyingi. Ambapo nakubali kuwa namna ya mafundisho iwe ni nzuri na ya kupatana na mpango wetu mzima, ni tumaini langu kuwaachia Serikali za Mitaa mzigo huu kabisa. Napenda kuwasihi wale wanaohusika na shule hizi, wakiwa ni TAPA au ni Wamissionari au Madiwani wa Serikali za Mitaa, waelewe kuwa wanashiriki katika kazi kubwa ambayo ni ya faida ya taifa zima, na washirikiane wapate kufanikiwa vizuri. Kwa upande wa shule za Sekondari, ambazo twaziweka mbele katika mipango yetu hivi sasa, ni lazima tutumie fedha zetu chache kuona kuwa tunatoa kwa haraka na kwa wingi hesabu kubwa ya waliopata School Certificate. Kwa kusudi hili ni lazima tukubali ubora wa shule za madarasa mengi (multi stream Secondary Schools) ingawaje hii itawakasirisha Serkali za Mitaa ambazo zina ndoto ya shule ya Sekondari katika wilaya yao. Tunaomba na tunapokea kwa mikono miwili misaada kutoka nchi za nje - misaada ya waalimu, misaada ya nafasi katika vyuo kwa masomo yale ambayo hayawezi kufundishwa humu Afrika ya Mashariki, na fedha kwa mipango mipya. Misaada ya fedha kama ule msaada uliofanywa na Agency for International Development kusaidia kujenga Chuo cha kufundishia Waalimu huko Chang'ombe, misaada toka sehemu nyingi kama vile tulivyosaidiwa katika kujenga University College Dar es Salaam, na misaada mingi kama vile ya waalimu kwa shule za Sekondari na Vyuo vya kufundishia waalimu, misaada yote hii tunahitaji sana. Misaada ya makampuni pia twaikubali, na tunawahakikishia kuwa nayo pia yapatana na mipango ya taifa letu.

## Shukrani

Kabla sijamaliza hotuba yangu, sinayo budi kuwakumbuka kwa shukrani watumishi wote wa elimu katika Tanganyika. Ni walimu wote katika shule za primary vijijini na mjini, waalimu katika Seconry Schools na vyuo vingine vyote, maofisa katika wilaya, mikoa, na afisi kuu hapa Dar es Salaam. Sisahau madiwani na wajumbe katika komitii na konseli za elimu za aina mbalimbali zinazoshughulikia elimu. Hili ni jeshi kubwa linalopambana naa dui yule Ujinga. Tunamtakia kila mmoja uhodari wa mahali anapotumikia.

**Mwishowe, tunaposherehekea kuchaguliwa kwa mheshimiwa Rais wetu kuwa Mkuu (Chancellor) wa kwanza wa Chuo Kikuu cha Afrika ya Mashariki na tukumbuke kuwa Rais wa baadaye, pengine hata wakati huu tunapozungumza, anajifunza, a, be, che, katika darasa la kwanza katika shule mojawapo ya kwetu ambayo imejengwa kwa bidii za watu wetu wenyewe na waalimu wake ni raia wa nchi hii wanaojitahidi kufundisha kwa ubora zaidi.**

Na tufanye tuwezavyo kuona kuwa namna ya elimu ambayo itamwongoza huyu kijana mdogo ni elimu ambayo watu wetu wataionea fahari,na ambayo hasa inafaa kwa kutoa viongozi wazuri wa nchi yetu kwa miaka mingi ijayo mbele yetu, elimu inayotupa watenda kazi hodari na wa aina nyingi, elimu inayojenga utu ulio fahari wa Kiafrika.

EAST AFRICAN PRINTERS TANGANYIKA LTD